**HOTUBA YA MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, AKIWA MGENI RASMI KATIKA MAADHIMISHO YA MIAKA 50 YA UHURU WA JAMHURI YA MSUMBIJI, MAPUTO TAREHE 25 JUNI, 2025**

Ni heshima kubwa sana kwangu kuungana nanyi kuadhimisha Miaka 50 ya Uhuru wa Taifa lenu. Sherehe hizi sio tu zinatukumbusha ushindi wa Msumbiji dhidi ya ukoloni, bali pia ni kielelezo cha ushirikiano, uvumilivu na mshikamano baina ya Waafrika.

Kwa msingi huo, ninakushukuru sana, Mheshimiwa Rais Chapo, kwa mwaliko wako kwangu kuungana na Marais wenzangu kushiriki katika tukio hili la kihistoria. Vilevile, mimi na ujumbe niliofuatana tunashukuru kwa ukarimu tuliofanyiwa tangu tulipowasili hapa Maputo.

Zaidi ya hayo, na kwa namna ya pekee, napenda kutumia fursa hii kukushukuru Mhe. Rais Chapo, kwa kunipa heshima hii adhimu ya kuwa Mgeni Rasmi, na kunipa fursa ya kuzungumza na ndugu zetu wa Msumbiji katika tukio hili kubwa na la kihistoria.

***Waheshimiwa Viongozi;***

*Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;*

Kuna methali inayosema, "**jirani anaposherehekea, kijiji kizima kinashereheka**." Tukiwa majirani na ndugu, uhuru wa Msumbiji, ni uhuru wetu, hivyo basi sherehe hizi za mikaka 50 ya uhuru ni fakhari yetu sote.

Kama nyote mjuavyo, Tanzania na Msumbiji si majirani tu waliotenganishwa na Mto Ruvuma, sisi ni ndugu wa damu. Udugu wetu uliimarishwa zaidi na waasisi wetu, Hayati Mwalimu Julius Nyerere wa Tanzania na Hayati Dkt. Eduardo Mondlane na baadae Hayati Samora Machel wa Msumbiji. Kupitia viongozi hao, wananchi wetu walifanya kazi bega kwa bega wakati wa harakati za ukombozi na hatimaye kuweza kupata uhuru wa Msumbiji tunaouadhimisha leo.

*Waheshimiwa Viongozi, Mabibi na Mabwana;*

Ni muhimu kufahamu kwamba, mbali na misingi ya kisiasa ya kutaka uhuru, haki na usawa, kulikuwepo sababu mbalimbali zilizofanya Tanzania ijihusishe katika harakati za ukombozi wa Msumbiji.

Mojawapo, ni imani yetu kuwa Afrika ni moja na waafrika ni ndugu zetu. Sio siri kuwa Watanzania na Wamsumbiji wana uhusiano

wa kihistoria na wa damu. Tanzania kuna Wamakonde, Wayao na Wamakua, kama ambavyo walivyo nchini Msumbiji. Katika kusisitiza uamuzi wa Tanzania kuunga mkono harakati za Ukombozi wa Taifa la Msumbiji, Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, aliitumia jamii ya Wamakonde kama mfano, nanukuu:

**"Mmakonde anayeishi Kaskazini mwa Ruvuma hana tofauti na Mmakonde anayeishi Kusini mwa mto huo. Kukataliwa uhuru kwa mmoja ni kukataliwa uhuru kwa wote wawili. Na Mmakonde aliyezaliwa kaskazini mwa Mto Ruvuma ni Mtanzania. Kumnyima uhuru wake ni kuwanyima Watanzania wote uhuru wao. Hakuna Mwafrika aliye huru wakati Waafrika wengine wanatawaliwa na ukoloni."** Mwisho wa kunukuu.

Sababu nyingine ni kuwa, uwepo wa ukoloni kwa Msumbiji ilikuwa ni tishio kwa uhuru wa Tanzania pia. Ni ukweli kuwa, watu wa Kusini mwa Tanzania siku zote waliishi kwa hofu kwa sababu ya vitisho na mashambulizi ya Wakoloni yaliyokuwa yakiongezeka. Uchokozi katika mpaka wa Kusini na Msumbiji uliilazimu Tanzania kuchukua hatua za kuunga mkono harakati za ukombozi za watu wa Msumbiji

Tanzania ilikuwa moja ya hifadhi kwa wakimbizi na wapigania uhuru waliokimbia Msumbiji, na kutafuta nafasi ya kujipanga vyema kukabiliana na Wakoloni. Hali hiyo ndio iliwezesha Chama cha FRELIMO kuanzishwa pale Dar es Salaam mwaka 1962.

Katika kuchochea matayarisho ya kupambana na kumng'oa mtawala dhalimu, Tanzania iliweka kambi za kuandaa mikakati na kutoa mafunzo ya kijeshi kwa wapigania uhuru wa Msumbiji. Kambi za aina hiyo zilikuwepo kwa upande wa Tanzania Bara na Zanzibar. Vilevile, Tanzania ilikuwa ndio Makao Makuu ya Jukwaa la Nchi za Mstari wa Mbele (Front line states), na mwenyeji wa Kamati ya Ukombozi ya Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU). Kamati hio ilikuwa inaratibu upatikanaji wa misaada kwa ajili ya wapigania uhuru wa nchi za Kusini mwa Afrika wakiwemo wa Msumbiji.

Hata baada ya kupata uhuru, Tanzania na Msumbiji tuliimarisha ushirikiano na mshikamano katika siasa za Afrika na kimataifa; katika zoezi la kujengeana uwezo, Ubalozi wa Msumbiji mjini Addis Ababa ulianza kwa kuendesha shughuli zake ndani ya Ubalozi wa Tanzania mpaka pale Msumbiji ilipoweza kupata jengo lake la Ubalozi.

***Waheshimiwa Viongozi Mliopo,***

***Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana;***

Ni wazi kuwa, Sherehe kama hizi za uhuru ni ukumbusho wa mapambano ya kutafuta uhuru, haki na usawa. Kwa hakika, ni katika nyakati kama hizi sisi kizazi cha sasa tunakumbushwa kuhusu namna wazee wetu walivyojitoa mhanga kwa ajili ya kupigania haki ya Waafrika kujitawala.

Harakati hizi ziliigharimu Msumbiji, na vilevile zilizigharimu nchi zilizokuwa mstari wa mbele kuiunga mkono, kama Botswana, Tanzania, na Zambia. Ndugu Sergio Vieira aliyekuwa Katibu wa Hayati Samora Machel alipata kusema kuwa: **'Tanzania ilifanya kitu cha kishujaa ambacho kisingeweza kufanywa na nchi nyingine. Kulikuwa na kambi Kongwa na Nachingwea, ambapo tulitoa mafunzo na kufanya lolote lile. Jeshi la Anga la Ureno lilikuwa likija kila wakati. Ilikuwa ni hatari. Baadhi ya ndege za Ureno zilitunguliwa hapa Tanzania; Zambia pia ilikabiliwa na tishio kama hilo la kivita wakati wote**.' Mwisho wa kunukuu. ('*Tanzania took a great risk that nobody could dare to take. There were camps in Kongwa and Nachingwea, where we could train and do anything over there. The Portuguese air force was coming all the time. It was a risk. Some Portuguese planes were*

*shot down here in Tanzania; Zambia too faced similar risk of war all the time.'*) Mwisho wa kunukuu.

Miundombinu mbalimbali ya Tanzania ilihujumiwa na kushambuliwa na wakoloni, ikiwemo maeneo ya kusini mwa Tanzania, na hata katikati ya Jiji kuu la Dar es Salaam. Hiki kilikuwa kipindi kigumu kiuchumi, ila nchi zilizosimamia ukombozi wa Kusini mwa Bara la Afrika walikuwa tayari kuchelewesha maendeleo yao kwa ajili ya kuhakikisha kuwa mapambano haya yanafanikiwa. Hivyo, leo tunaposhuhudia ndugu zetu wa Msumbiji wakisherehekea Miaka 50 ya Uhuru wao, nasi ndugu zenu Watanzania tunashereheka pia. **Ushindi wa Msumbiji ni ushindi wetu, mafanikio ya Msumbiji ni mafanikio yetu pia, na maendeleo ya Msumbiji ni maendeleo yetu sote.**

**Mheshimiwa Rais,**

Baada ya kupata uhuru wake, Msumbiji ilikuwa mstari wa mbele kuunga mkono mataifa mengine, yakiwemo Zimbabwe, Afrika Kusini na Namibia, hatua iliyoharakisha mafanikio ya mapambano kwenye nchi hizo. Hivyo, nitumie fursa hii kuipongeza Serikali ya Msumbiji na wananchi wote kwa mchango wao mkubwa kwenye harakati za ukombozi wa Bara la Afrika.

Tanzania leo, inaungana nanyi kutoa heshima kwa mashujaa wote wa Msumbiji, wanawake kwa wanaume, kwa kujitoa kwao muhanga katika vipindi vigumu vya harakati za ukombozi. Kwa upande mwengine, Tanzania pia tunakumbuka msaada wa hali na mali tuliopata kutoka kwa Msumbiji Huru mwaka 1978 na 1979 kufuatia vita na Nduli Idi Amin wa Uganda alipovamia Tanzania. Hivyo, pamoja na shukurani tulizozitoa wakati ule, leo kwa mara nyengine tena natoa shukrani zetu kwa msaada wenu wa kutusaidia kulinda nchi yetu pia.

**Waheshimiwa Viongozi,**

**Mabibi na Mabwana;**

Tunaposherehekea miaka 50 ya Uhuru wa Msumbiji, nitumie fursa hii kuipongeza Serikali na Wananchi wa Msumbiji kwa mafanikio makubwa mliyoyapata katika kipindi hiki cha nusu karne iliyopita. Kwa hakika, kupitia umoja, kujituma na dhamira njema isiyotetereka, Msumbiji imeinuka kutoka kwenye kivuli cha ukoloni na kujenga mustakabali mpya wa uhuru, heshima na ustawi wa pamoja kwa raia wake. Kwa namna ya pekee, napenda kuwapongeza wote, wakiwemo

Viongozi waliopita kwa mafanikio haya. Hongereni sana, **na nimefurahi kuwaona wote wapo hapa (Mzee Chisano, Mzee Gwebuza na Kaka yangu Filipe Nyusi)**.

Ninaamini chini ya uongozi mahiri wa Rais Daniel Chapo, watu hodari wa Msumbiji wataendelea kupiga hatua kubwa za maendeleo. Na ninataka nikuahidi kuwa, Tanzania itaendelea kuwa nawe bega kwa bega katika kusukuma mbele gurudumu la maendeleo.

Aidha, katika kuzidi kufungua fursa zaidi za biashara baina ya wananachi wa Msumbiji na Tanzania, ninayo furaha kueleza kuwa, Shirika la Ndege la Tanzania linatarajia kuanza safari za ndege kati ya Tanzania na Msumbiji mwisho wa mwaka huu, hatua itakayoimarisha uhusiano wa kibiashara na kiuchumi baina ya watu wetu.

**Waheshimiwa Viongozi,**
**Mabibi na Mabwana;**

Bara letu limefanikiwa kwa kiwango kikubwa katika hatua ya kwanza ya ukombozi, yaani uhuru wa kisiasa. Tunapaswa kuhakikisha kuwa nchi zetu zinakuwa na amani na umoja wa kitaifa, ili tuweze kushirikiana kufanikisha hatua nyingine za mageuzi ya kifikra, na kutafuta uhuru wa kiuchumi.

Katika hili, hatua mojawapo ni kuhakikisha tunaunganisha watu na kuleta umoja wa Kitaifa. Katika sherehe hizi tumeshuhudia uwepo wa Mwenge wa Uhuru, mwenge ambao umetembezwa nchi nzima kwa nia ya kuwaleta watu pamoja na kuamsha ari ya mshikamano na uzalendo. Niwaombe kuendeleza jitihada hizi, kwani kupitia mwenge huu, heshima na matumaini ya wananchi yanakwenda kuamshwa. Jitihada hizo ziende sambamba na kuhakikisha kwamba wananchi wanakuwa na imani na nchi yao, waweze kutanguliza maslahi ya nchi kabla ya kwao wenyewe, kulinda na kuhifadhi rasilimali za nchi kwa ajili ya maendeleo na ustawi wa wananchi. Katika kufanya hivyo, kuna haja ya kumuinua mwanamke kama nyenzo muhimu ya maendeleo ya kiuchumi, kisiasa na kijamii.  Ni kwa sababu hiyo, ninawapongeza sana kwa kuchagua kaulimbiu ya mbio za Mwenge wa Umoja wa Kitaifa za mwaka huu isemayo **Miaka 50: Kuwainua Wanawake, Kujenga Usawa wa Kijinsia** ("*50 Years: Empowering Women, Building Gender Equality*"). Hayati Samora Machel alipata kuzungumzia mapambano ya uhuru akisema kuwa "**Ukombozi wa wanawake sio jambo la hisani, linalotokana na fikra, huruma au msaada wa kibinadamu. Ukombozi wa mwanamke ni kiini cha kuleta mapinduzi, kwa maendeleo endelevu na ni sharti la msingi la kufanikiwa kwa mapinduzi**

**yenyewe**." (*"The Emancipation of women is not an act of charity, the result of a humanitarian or compassionate attitude. The liberation of women is a fundamental necessity for the revolution, a guarantee of its continuity and a precondition for its victory*.")

Ni fahari kutambua kwamba, licha ya mtazamo hasi kuhusu nafasi ya mwanamke kwenye jamii katika miaka ya 1960, wanawake wa Msumbiji waliweza kujitolea kuwa mstari wa mbele kwenye mapambano ya uhuru wa nchi yao. Kikosi cha Wanawake (*Female Detachment*) cha FRELIMO kilichoanzishwa mwaka 1967, kiliwezesha wanawake nao kushiriki mapigano. Hatuna budi kuwatambua wanawake waliochangia harakati za ukombozi, ambao wanaingia katika vitabu vya historia. Wanawake kama Josina Muthemba Machel, Paulina Mateus Nkunda, Filomena Likune, Filomena Nashake, Marina Pachinuapa, Mônica Chitupila, na wanawake wengine wengi, ambao walishiriki sio tu kupigania uhuru wa Msumbiji, bali pia kumuinua mwanamke kutoka aina zote za ukandamizaji.

Wanawake hao na wenzao, wanatukumbusha umuhimu wa kuendelea kuwekeza katika ustawi na maendeleo kwa jamii ya wanawake, ikiwemo upatikanaji wa huduma za afya, maji, elimu na

umeme (nishati safi). Katika hilo, niwapongeze sana Viongozi na wananchi wa Msumbiji kwa hatua kubwa zilizochukuliwa, kama ile ya kuwekeza kwenye miundombinu na huduma za afya zilizochangia kupungua kwa vifo vya mama wajawazito na watoto wakati wa kujifungua.

Vilevile, hatuna budi kuendelea kuchukua hatua kuwawezesha wanawake na vijana kunufaika zaidi na fursa zitokanazo na utangamano wa kikanda na soko la Afrika kwa ujumla. Umoja wa Afrika umepitisha Itifaki ya *AfCFTA* ya Wanawake na Vijana kwenye Biashara inayolenga kujibu baadhi ya changamoto zinazoyakabili makundi haya na kuyazuia wasifaidike na fursa zinazotengenezwa na soko la kikanda.

**Mheshimiwa Rais Chapo,**

Leo ni siku adhimu, ambapo kama nilivyosema awali, kijiji kizima kimekuja kushereheka kwa pamoja nanyi ndugu zetu, majirani zetu wa Msumbiji. Maadhimisho haya yawe chachu ya kuendeleza ushirikiano na mshikamano kwa watu wa Msumbiji bila kujali kabila na anakotoka. Vilevile, baina ya Waafrika wakati tunapoangazia njia za kuleta maendeleo endelevu na ustawi wa jamii zetu.

Kwa kuhitimisha, nimshukuru tena Mheshimiwa Rais Daniel Chapo, Serikali na Wananchi wa Msumbiji kwa ujumla, kwa kutimiza miaka 50 ya uhuru, na kwa maandalizi mazuri ya sherehe hizi. Nawatakia kila lenye kheri na mafanikio, katika kujenga umoja wa Taifa la Msumbiji.

**Mungu ibariki Msumbiji, Mungu Ibariki Afrika.**

**Asanteni sana kwa kunisikiliza.**

**Omti brigado.**